MKATABA WA AJIRA

Mkataba huu umeafikiwa leo, tarehe ….. mwezi ……., 2020, kati ya……...wa S.L.P ……., ARUSHA (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja.

NA

Ndugu ……...wa S.L.P……. ARUSHA (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mwajiriwa") kwa upande mwingine.

Kwakuwa mwajiri amedhamiria kumuajiri mwajiriwa na mwajiriwa yuko tayari kutimiza masharti ya mkataba huu kwa nafasi ya ……..…..…..kwa masharti na makubaliano yafuatayo;

Mkataba wa kazi utaanza tarehe ……mwezi……...na utadumu kutokana na makubaliano kati ya Mwajiri na Mwanga Children foundation

1. **MAJUKUMU:**
   - Kufundisha masomo watakayo pangiwa na kuwalea Watoto
   - Majukumu mengine atakayopangiwa na mwajiri wake.

2. **MASAA YA KAZI:**
   - Mwajiriwa atafanya kazi kwa masaa tisa ya utendaji wa kazi zake.

3. **MSHAHARA NA MASLAHI:**
   - mwajiri atamlipa mwajiriwa allowance kila mwezi kulingana na hali ya uchumi ya kituo
   - malipo haya yatajumuisha nauli na posho tu kama itakavyopangwa na mwajiriwa

4. GHARAMA NYINGINEZO:

- garama za likizo na uzazi hazitalipwa na mwajiri kwani hakuna makubaliano ya ajira rasmi kati ya pande zote mbili

5. USITISHWAJI WA MKATABA.

- Endapo mwajiriwa ataamua kuacha kazi, atatakiwa kumpa taarifa mwajiri taarifa ya miezi mmoja(Miezi 1) kabla.

- Endapo mwajiri ataamua kusitisha ajira ya mwajiriwa, atatakiwa kumpa mwajiriwa taarifa isiyozidi miezi mmoja (Miezi 1) kabla.

6. MAHALI PA AJIRA :

Mahali pa kazi itakua ni Arusha tindgani kata ya kimandolu

MASHARTI MENGINE

- Muajiri hatajihusisha kwavyovyote vile wakati wa akiwa ndani ya mkataba huu na biashara na mtu yeyote au kampuni inayohusiana na yamwajiri ndani ya Africa mashariki.

- Muajiriwa atatakiwa kutii, kutozembea katika kutekeleza maagizo yeyote kutoka kwa muajiri.

- Muajiriwa atatakiwa kuwa na mienendo mizuri wakati wowote katika mambo yake binafsi na yale ya kijamii ili asikidhalilishe kituo.

- Muajiriwa atatakiwa wakati wowote akiwa kazini au popote kuwa na tabia zinazoendana na utaratibu na maadili ya kituo

- Muajiriwa atatakiwa kutunza mali zote zinazo milikiwa na kituo au alizokabidhiwa.

- Muajiriwa haruhusiwi kutumia mali yoyote ya kituo kwa matumizi yake binafsi au kwa faida yake binafsi.

- Mkataba wa muajiriwa utakapositishwa na muajiri, muajiriwa atatakiwa kukabidhi mali zote zinazohusiana na kituo alizokuwa amekabidhiwa.

- Muajiriwa yeyote anayefahamu mtu yeyote anayekitendea kituo uhalifu wa aina yoyote au anakwenda kinyume na taratibu au masharti ya mkataba, muajiriwa atatakiwa kutoa taarifa kwa mkuu wa kitengo kwa maandishi.

Kwa muajiriwa kukubali ajira hii, Itamaanisha kuwa muajiriwa anampa jukumu muajiri la kulinda hatimiliki za kazi zinazotokana na ajira ya muajiriwa wakati wa ajira yake.

MAKUBALIANO:

Makubaliano katika mkataba huu yanachukuliwa kwamba Mwajiri ameusoma na kuuelewa mkataba huu kabla ya kuuingia.

Umesainiwa Arusha leo tarehe……mwezi wa …….. 2020.

…….. **……..**

Shahihi kwaniaba ya Mwajiri. **Sahihi ya Mwajiri**

Mbele yangu

Jina :……

Cheo:…….

Saini: ……..